



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**



Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na KMC/M10/52/108

30 Oktoba, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Shirika lisilo la Kiserikali la Tanzania Health Promotion Support (THPS) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama linapenda kuwatangazia Umma juu ya nafasi za kazi katika vitengo mbalimbali kama ifuatavyo;

I. MTOA HUDUMA ZA UPIMAJI WA VVU KATIKA JAMII.

(COMMUNITY HIV TESTING) NAFASI (3)

Kituo Busoka, Mwime, Mwendakulima.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya Cheti cha Uuguzi na Ukunga (Certificate of Nursing), Diploma ya Utabibu (Diploma in Clinical Medicine), Diploma ya Huduma ya Maabara (Diploma in Laboratory Technician)
- Awe na Uzoefu wa Huduma za Tiba na Matunzo
- Awe na Leseni ya Taaluma Husika.

II. MTAKWIMU: Nafasi (1) – KITUO IYENZE

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya Stashahada ya Records (Diploma in Records/IT/Computer Science/Statistics)
- Awe na Uelewa wa kutumia kompyuta.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, 81Boma Road, 37305 MALUNGA, S.L.P 472, KAHAMA, SHINYANGA
Barua pepe: info@kahamamc.go.tz /md@kahamamc.go.tz Tovuti www.kahamamc.go.tz

III. CLINICAL TRACKER: Nafasi (1) KITUO NGOGWA

SIFA ZA MWOMBAJI

- Mhudumu wa Afya (Medical Attendant)
- Community Health Walker
- Diploma in Social Work
- Diploma in Community Development

IV. ART NURSE (MUUGUZI HUDUMA YA DAWA ZA ARVs) Nafasi (1) KITUO NYAMBULA

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya Cheti cha Uuguzi na Ukunga
- Awe na Uzoefu wa huduma za Tiba na Mafunzo
- Awe na Leseni

V. CTC SITE MANAGER (MSIMAMIZI KITENGO CHA TIBA NA MAFUNZO) Nafasi (1) KITUO HOSPITALI YA MANISPAA KAHAMA

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Shahada ya Udaktari wa Binadamu
- Awe na stashahada ya Utabibu
- Awe na Uzoefu wa Huduma za Tiba na Matunzo
- Awe na Leseni ya Taaluma Husika

VI. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si Zaidi ya Miaka **45** na sio pungufu ya Miaka **18**.
- ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.


Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, 81Boma Road, 37305 MALUNGA, S.L.P 472, KAHAMA, SHINYANGA
[Barua pepe:info@kahamamc.go.tz](mailto:info@kahamamc.go.tz) /md@kahamamc.go.tz Tovuti www.kahamamc.go.tz

- iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.
- v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa
- vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- vii. Waombaji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni
- viii. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 12 Novemba, 2024 Saa 9:30 Alasili.
- x. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
KAHAMA – SHINYANGA

- xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na;


Masudi Kibetu
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
KAHAMA

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, 81Boma Road, 37305 MALUNGA, S.L.P 472, KAHAMA, SHINYANGA
Barua pepe: info@kahamamc.go.tz /md@kahamamc.go.tz Tovuti www.kahamamc.go.tz